

TANGAZO LA SERIKALI NA. 656 la tarehe 18/11/2022

SHERIA YA UMEME,

(SURA YA 131)

—  
**AMRI**  
—

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha. 23 na 24)*

AMRI KWA AJILI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA YA UMEME KWA KAMPUNI YA  
WATU NA UMEME TANZANIA LIMITED YA MWAKA 2022

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri kwa ajili ya kurekebisha bei za huduma ya Umeme kwa Kampuni ya Watu na Umeme Tanzania Limited ya mwaka 2022.

Marekebisho ya bei

2. Bei za Umeme kwa ajili ya Kampuni ya Watu na Umeme Tanzania Limited zilizoainishwa katika Jedwali la Amri hii zimeidhinishwa.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

- (a) ifikapo tarehe 31 Machi, 2023 au kabla, Watu na Umeme Tanzania Limited itawasilisha katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa;
- (b) ifikapo tarehe 30 Juni, 2023 au kabla, Watu na Umeme itatayarisha na kuwasilisha kwa Mamlaka ilikuidhinishwa Mkataba wake wa

*Amri Kwa Ajili ya Kurekebisha Bei Za Huduma ya Umeme Kwa Kampuni ya Watu Na Umeme Tanzania*

*Tangazo la Serikali na. 656 (linaendelea)*

Huduma kwa Wateja;

- (c) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi 2023, Watu na Umeme wawe wamebadili mfumo wamanunuzi ya umeme kuwezesha ununuzi kwa unit ikwa shilingi. Aidha, wateja waweze kuona matumizi ya unit izilizotumika;
- (d) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi, 2023, Watu na Umeme ihakikishe mita mbovu zote za wateja zimekarabatiwa au zimebadilishwa na pia mita zinapatikana kwa matumizi ya baadaye.
- (e) Kila robo mwaka, Watu na Umeme itaendelea kuwasilisha katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

**BEI ZILIZOIDHINISHWA**

Kundi la Wateja	Bei Zilizoombwa			Bei zilizoidhinishwa		
	Matumizi (Uniti kwa Mwezi) - kWh/Mwezi	Bei Inayoombwa kwa Unit (TZS/kWh)	Bei inayoombwa kwa Mwezi (TZS/Mwezi)	2022/23(TZS/kWh)	2023/24 (TZS/kWh)	2024/25 (TZS/kWh)
Majumbani (Kawaida)	8.25	1,333	11,000	1,306	1,306	1,306
Majumbani (Kati)	16.5	1,212	20,000	1,086	1,086	1,086
Biashara/Taasisi za Umma	33.0	970	32,000	941	941	941
Uzalishaji	49.5	889	44,000	801	801	801

*Amri Kwa Ajili ya Kurekebisha Bei Za Huduma ya Umeme Kwa Kampuni ya  
Watu Na Umeme Tanzania*

*Tangazo la Serikali na. 656 (linaendelea)*

**GHARAMA ZA MAUNGANISHO ZILIZOIDHINISHWA**

Makundi ya Wateja	kiasi	Gharama iliyopendekezwa	Gharama Iliyoidhinishwa
Majumbani (kawaida)	TZS/connection	100,000	27,000
Majumbani (kati)	TZS/connection	100,000	27,000
Biashara / Taasisi	TZS/connection	100,000	100,000
Productive	TZS/connection	100,000	100,000

Dodoma.  
....., 2022

MODESTU M. LUMATO  
*Mkurugenzi Mkuu*